

FORM FOUR TERM ONE EXAM 2017

KISWAHILI
Karatasi 3
Lugha
Muda: Saa 2 1/2

SCHOOLS NET KENYA
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

Karatasi hii ina kurasa 3 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

**SEHEMU A: USHAIRI
SWAL LA LAZIMA**

1. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

Ajaye kisimani mbele, hunywa maji maenge,
Asinywe yalo na vunju,
Yakampa kigegezi
Yakamtibua roho akaona na kinywa,
Awali ndio awali mbovu hamna

Ikiwa utalimatia,
Utayaramba makombo,
Uvidata vitucheche,
Kisoma aali kikupe kisogo
Inajuzu ujihimu
Mwanafuu darasani
Uraukapo bukrata
Katu hutayaramba makombo
Hutokosa kisebeho.

Dereva nawe utingo,
Natija ni asubuhi,
Wateja utawawahi,
Wasaa kuzingatia,
Uwafikishe kazini,
Kwa wasaa ufaao,
Wasije wakateteshwa na
Bosi wao nao wakuapize

Nawe mwanazaraa,
Mpini uukamate kabla,
Jua kutiririsha majasho jasadini,
Ushindwe kung'oa magugu,
Kutoka kwa lako konde.

Mhadimu mwenye zohali,
Yajuzu ujihimu
Maziwa ununue majogoo
Usije ukayadata na hivyo
Ukaandaa chai mkandaa
Wateja wakuambae mithili ya ibilisi

MASWALI

- (a) Shairi ni la aina gani? Eleza (alama 2)
- (b) Eleza nasaha yoyote inayotolewa kwa wafanyikazi wowote watatu (alama3)
- (c) Je, wafanyikazi waliolengwa na mshairi wataathirika vipi endapo hawatafuata ushauri wanaopewa kwenye shairi? (alama 3)
- (d) Kwa mujibu wa mshairi, mwanafunzi anahimizwa kurauka mapema kwa nini ? (alama.2)
- (e) Tambua tamathali zozote mbili za usemi zilizotumiwa na mtunzi (alama.2)
- (f) Taja sifa zozote mbili za kimuundo zilizotumiwa na msanii (alama.2)
- (g) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari (alama.3)
- (h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi (alama.2)
- (i) Wakuapize
- (ii) jasadini
- (i) Onyesha matumizi yoyote ya mstari mshata

SEHEMU YA B

Riwaya-Kidagaa kimemwozea

2. “Nini hii? What is this?”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Eleza masaibu ya kinachoashiriwa (alama.8)
- (c) Taja na ufafanue mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili (alama.4)
3. “Mchimba kisima huingia mwenyewe” Jadili kauli hii ukirejelea riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (alama 20)

SEHEMU YA C. Mstahiki Meya-Timothy M.Arege

4. “Mwondoe huyu mara moja!”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Eleza yanayomfanya msemewa kufukuzwa (alama.8)
- (c) Eleza sifa **nne** za msemewa (alama.4)
- (d) Msemaji anaamua kufanya nini kutokana na mazungumzo haya. (alama.4)

5. “Unafiki ni mojawapo wa sababu za kuwepo uongozi mbaya katika mji wa Cheneo” Thibitisha kauli hii (alama.20)

SEHEMU YA D

Hadithi fupi: Damu Nyeusi na Hadithi nyingine

Mke wangu

6. “.....si nitaonekana nina wazimu.....kila mtu na kazi yake”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili? (alama.4)
- (b) Ukirejelea sifa za msemewa, thibitisha ukweli wa methali umdhaniye ndiye, siye” (alama.6)
- (c) Eleza sifa **tano** za Aziza (alama.5)
- (d) Ni sababu zipi zinazomfanya Aziza kuomba talaka (alama.5)
7. Ukirejelea hadithi ya “***Mke wangu, Samaki wa Nchi za Joto, Damu Nyeusi na Gilasi ya Mwisho Makaburini***, eleza alivyosawiriwa mwanamke (alama.20)

SEHEMU YA E

Fasihi simulizi

8. (a) (i) Eleza maana ya mawaidha katika fasihi simulizi (alama.2)
- (ii) Fafanua sifa zozote **nne** za mawaidha (alama.4)
- (b) Eleza umuhimu wa ngomezi (alama. 10)
- (c) Taja sifa **mbili** za bembelezi (alama.4)